*Abstract of Faith (Kiswahili)*



# Misingi Ya Imani

**Zion Assembly Church of God**
**International Offices**

**Mailing Address:**
P.O. Box 2398
Cleveland, Tennessee USA 37320

**Location:**
5512 Waterlevel Hwy
Cleveland, TN USA 37323

***Zion Assembly Church of God***
***Publishing House***

**Reprinted Oct. 2018**

# ZION ASSEMBLY

## CHURCH OF GOD

# MSINGI YA IMANI.

## DIBAJI

'Zion Assembly Church of God' ni Kanisa la kiroho yenye waumini waliokubalianana na Mungu  na kutii mafundisho ya Kristo na mitume wake (kutoka 19;3 –16. Yohana14:6,8,14; Matendo 2:42; Waefeso 5:24-32). Msimamo huu ni thabiti hata katika wakati huu wa uasi ambapo wengi "hujitenga" na (kuondoka) katika imanill (2 Wathesalonike 2:1 -12; 1Timotheo 4:13; 2 Petro 2; 3:1 -12; Yuda 3 -19).

Wahudumu na washiriki wa 'Zion Assembly' wamekubali na kuishi na kuabudu pamoja katika "imani hii takatifu, kutembea katika ukweli, "kujitahidi kuhifadhi umoja wa kiroho kwa ufungamano wa amani," na utakakatifu kati yao. 'Wao hutafuta ukamilifu wa Kristo katika ushirika wao, na kwa neema na nguvu zake sawasawa na mfano wa Yesu Kristo kiasi kwamba akionekana watakuwa kama yeye kwa mfano wake (Warumi 8:29; 'Wakolosai 1:1-17; 1Yohana3:2).

Mbali na msukumo huu wa kindani ya kukuza upendo na ulinzi ndani ya nyumba nzima ya Mungu, wahudumu na washiriki wa 'Zion Assembly' wamechukua jukumu ya kuhakikisha umoja wa waumini wote mpaka wote waone "uso kwa uso," "waseme kitu kimoja," na" kutembea chini ya sheria moja" (Isaya 52:8, lWakorintho 1:10; wafilipi 3:16). Kwa njia hii wanatafuta kuendeleza maneno ya mitume: Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu, na kuwa mtu mkamilifu hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo (Waefeso 4:13) .

## KUWA MSHIRIKA WA KANISA.

Kuwa mshirika wa 'Zion Assembly' u wazi kwa waumini wote ambao ushuhuda wao umethibitishwa kwa matunda ya kuzaliwa upya na waliotayari kufanya agano pamoja na Kristo na Kanisa kutembea katika nuru ya injili. Wanaonuia kuwa washirika wataungama hivi:

"Je una ahidi kwa dhati mbele za Mungu na mashahidi hawa kwamba unakubali Biblia hii kuwa ni neno la Mungu, kuamini na kutenda mafundisho katika halali yake, na Agano jipya kama mwongozo wako wa imani na tendo, ufalme na nidhamu, na kukubali kutembea pamoja kama mwili mmoja katika nuru ya injili kwa ukamilifu na uwezo wako wote?"

Katika kuitikia mwongozo huu wa agano anayenuia kuwa mshirika hujibu: "Kwa neema ya Mungu nimekubali." Baadaye mshirika mpya atawekewa mkono na mhudumu ambaye atamwombea uongozi na nguvu za mungu; waumini hufuata kwa makaribisho ya upendo, na kumnyooshea mkono wa kuume wa ushirika.

**MAFUNDISHO MUHIMU KATIKA MAANDIKO**

**Tanbihi**: Matamshi haya hayajanuiwa kuunda aina ya imani ama kufikiriwa kueleza kinagaubaga Misingi ya imani ambalo kwalo Kanisa limejengwa. Ni baadhi ya mafundisho muhimu na kanuni zilizoko kwenye maandiko matakatifu yanayofanya sehemu muhimu ya uongozi wa imani Kanisani.

**Utatu wa Mungu** - Biblia hufundisha kuwa Mungu moja wa milele hudumu katika u tatu; Baba, Mwana, na Roho mtakatifu. Watatu hawa wanamiliki sifa zao kila mmoja mwenyewe na bado wanaungana pamoja kuwa Mungu mkuu wakiwa kwenye umbo moja. (Warumi 5:5; 15:16; 30,2 wakorintho 1:20; 5:19; Yohana 3:5; Waefeso 2:18; 3:5), Baba ni Mungu (Waefeso 4:6) Mwana ni Mungu (Yohana 1:1-3 10:1,Waebrania 1:8 Ufunuo 1:8) Roho Mtakatifu ni Mungu (Yohana 14:17,16:13; Matendo 5:3; Wakorintho 2:10) na sio miungu mitatu bali Mungu mmoja. Utatu mtakatifu hufanya kazi pamoja katika umoja ulio wa utimilifu kwa wokovu wa mwanadamu (Yohana 3:5,6:44; 16:17; 2 Wakorintho 5:19).

**Yesu Kristo** - Yesu Kristo ni "mfano wa Mungu asiyeonekana"(Wako1osai 1:15) na "mwana wa pekee wa Mungu" (Yohana 3:16). Katika yeye Mungu alijidhihirisha katika mwi1i, akajulikana kuwa ni haki katika Roho, akaonekana na malaika, akahubiriwa katika ulimwengu, akachukuliwa juu katika utukufu na sasa anakaa katika mkono wa kuume wa Mungu akituombea (Matendo 7:55, 1 Timotheo 3: 16). Kupitia kwake pekee watu humfikia Baba wa mbinguni. Ni kupitia kifo chake iletacho upatanisho ndio tunaokoka. "wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu waliopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo"(Matendo 4:12). Yeye asiye na mawaa ndiye "mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi za ulimwengu" (Yohana 1 :29). Kama kristo naye ni kichwa cha Kanisa naye ni mwokozi wa mwili (Waefeso 5:23).

**Biblia** - Maandiko matakatifu - Agano la kale na agano Jipya hufunua Mungu na mapenzi yake kwa binadamu. Ni pumzi ya Mungu usio na upotovu, kosa, wala hayawezi kubadilishwa (2Timotheo 3:14 - 16; 2 Petero 1:16-2.1). Ukweli wa maandiko umefunuliwa kwa unabii, kivuli, mifano, na kuangazwa kupitia nguvu za Roho mtakatifu. Mafundisho ya biblia - hasa katika nuru ya Agano Jipya ndiyo utawa1a wa mwisho wa imani ya Kanisa, matendo, ufalme na nidhamu (Matendo 2:42, 2 Petro 3:12). Kutembea katika nuru va neno 1a Mungu ndio mwongozo wa maadili na juhudi ya Kanisa la Zion Assembly. "Neno lako ni taa kwa miguu yangu na mwangaza wa njia yangu" (Zaburi 119:105).

**Kanisa** - Kanisa ni mwili unaoonekana wa waumini unaoundwa na kuunganishwa kwa kufanya agano na Mungu kutii sheria zake (Kutoka 19:5 - 8; 24:3 - 8; Zaburi 119:57; Yohana 14:15, 17:6,8,14; 1Petro 2:9). Yapatikana chini ya uongozi wa Mungu unaotowa sheria na mwongozo kupitia kwa Roho na maandiko kwa watu wa Mungu (Isaya 2:2 -

4;9:7; Mathayo 18:15 - 20 1 Wakorintho 12:28). Kwa sasa, Kanisa ha1ijakamilika, lina mawaa na wanaorudi nyuma na 'wandugu bandia' ( Wakorintho 5; Waga1atia 2:4; Yuda 4). Ni tofauti basi na ufa1me wa Mungu ambao ni uongozi wa kiroho kwa waumini wote waliozaliwa upya (Yohana 3:3 - 8; warumi 14:17;Wako1osai 1:13). Mmoja 'anazaliwa' katika ufalme na 'kuongezewa' kanisani (Yohana 3:3-8; Matendo 2:47). Kanisa litafaulu kutangaza injili kote ulimwenguni (Mathayo 24:14;28:18 - 20, Mariko 16:15 -, 16); itakami1ika ' kwa kuoshwa na maji kwa neno' na itakabidhiwa kwa Kristo katika utukufu na utakatifu wake ( waefeso 5:26,27). Mkutano Mkuu ndicho kina mamlaka ya kutafsiri maandiko kwa kanisa (Matendo 15;16:4,5). Kusudi 1a mkutano Mkuu ni kuendeleza umoja na ushirika kati ya waumini; kutafuta maandiko ili kusuluhisha tofauti ya ufarisi unaoleta kutenganisha watumishi na makanisa. Mambo yote yanayohusiana na uongozi na nidhamu hujadi1iwa na kutatuliwa mbele ya waumini katika umoja kwa kumtii Roho mtakatifu (MS 12,22,28), "Kwani imempendeza Roho mtakatifu kwetu'. Washirika wote waume waliosimama imara wana sauti kwenye kikao. Wamama ni sehemu muhimu katika huduma. Hata hivvo kwa mambo ya mamlaka ya kanisa wanatoa maoni yao kupita kwa waume zao na wazee wa kanisa ( lWakorintho 11:3,7-9:14:34-36; Timotheo 2:12;13-17)

**TENDO LA WOKOVU WA NEEMA**.

**Kuhukumiwa** - ni Ufunuo wa Roho mtakatifu kwa binadamu kuhusu hukumu ya haki wa Mungu. Wale ambao hawajafanywa upya rohoni hujiona watenda dhambi mbele za Mungu huhisi kosa na kuelewa kutenganishwa na aliye mtakatifu mwenye haki na aliye mwema (Isaya 6: 1; Yohana 6:44; Matendo 2:3738), Toba ya kweli inafanywa tu kupitia kwa kazi ya Roho ya kushtaki
(Yohana 16:7 – 15; 1 Wakorintho 12:3; Yohana 8:32; 14:6).

**Toba** - ni tendo 1a mtu kuungama dhambi zake mbele za Mungu baada ya kukubali kuziacha na kumrudia Kristo kwa moyo, akili, nafsi na nguvu zake zote.Toba ya kweli inafanywa tu katika huzuni wa Kiungu (2 Wakorintho7:9.10) Toba inadhihirishwa kwa matunda 'yapasayo toba' (Mathayo3:8;Warumi 6:2).Tendo la toba hufuatwa na ubatizo wa maji (Taz Mariko 1:4,5,15 Luka 13:3;Matendo 3:19;5:30,31:1Yohana 1:9).Toba ni lazima ili mtu ahesabiwe haki.

**Kuhesabiwa Haki** - ni hali ya mtu kutokuwa na kosa mbele za Mungu. Hii yawezekana kupitia damu ya upatanisho ya Yesu Kristo. Ni tendo la msamaha kwa mwenye dhambi sugu aliyebadilika. Kuhesabiwa haki ni matokeo ya toba na imani (Warumi 8:1-2; 3:23-26; 1 Yohana 1 :7). Mtu aliyehesabiwa haki ana 'Amani kwa Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo (Warumi 5:1.2). Kuhesabiwa haki hudhihirisha msamaha: namna ya kuzaliwa upya.

**Kufanywa Upya** - ni tendo la Mungu la kuumba maisha mapya moyoni mwa muumini kupitia Roho Mtakatifu. Ni jambo la hakika Iinalotendeka papohapo. Binadamu amekufa katika dhambi na uhalifu wa Adamu, na waweza kuhuwishwa tu kupitia imani ndani

ya Kristo na damu yake ya upatanisho (Waefeso 2:1- 45:Wakolosai 2: 13,14: Yohana 5:24). Kufanywa upya ni sawa na kuzaliwa upya;hali yakuzaliwa mara ya pili.

**Kuzaliwa mara ya pili** - ni tamko nyingine ya kuzaliwa upya. Matokeo ya tendo hili ni kuumbwa upya ambapo mwumini hufanyika mwana wa Mungu. Kupitia kuzaliwa upya, mtu anafanywa sehemu ya ufalme wa Mungu. Yesu aIisema; 'lazima uzaliwe mara ya pili' (Yohana 3:3 - 8; IPetro 1:23). Kuzaliwa upya ni hitaji 1a kwanza ili utakaso uonekane.

**Tunda la Roho** -Ina asili ya kiungu. Ni uhai ule wa Mungu unaomwagwa moyoni mwa mtu aliyefanywa upya. Tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumihvu, utu wema, fadhili, uaminifu (Wagalatia 5:22,23). Tunaambiwa katika maandiko kutembea katika Roho wala tusiyatimize tamaa za mwili (Waga1atia 5:16; Waefeso 5:7 Wafilipi 1:11).

**Uponyaji wa kiungu** – umewekwa kwa wote walio katika upatanisho. Dhabibu ya upatanisho ya Kristo msalabani unaleta uponyaji hata kwa mwili wa mwanadamu. Uponyaji wa kiungu unatokana na imani pasipo usaidizi wa dawa wa1a ujuzi wa upasuaji. Pakitokea kisa ambapo mtu ameponywa kwa usaidizi wa madaktari, dawa,miti shamba n.k, Mungu bado anastahili kusifiwa; kwani Mungu ndiye anaponya katika njia yoyote ile. 'Bariki Bwana, ee nafsi yangu! Wala usisahau faida zake. Anaye kusamehe maovu yako yote; anayaponya magonjwa yako yote' (zaburi 103:2,3;) Isaya 53:4,5; Mathayo 8:17; 2Petero 2:24; Yakobo 5:14 -16).

**NEEMA YA ZIADA.**

**Utakaso** - ni kazi halisi ya pili ya neema inayoletwa moyoni mwa mtu aliyefanywa upya kwa imani. Katika utakaso, utu wa asili unaondolewa(Waebrania 10:10; 13: 12, 13; Warumi 6:1-6: 1Wathesalonike4:3: 2Wathesalonike2:13;.lPetero 1:2) .. Utakaso humwezesha mwumini kuleta mwili wake chini ya uongozi wa Kristo na kulingana na neno la Mungu. Utakaso ni lazima, kisha hufuatwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu.
Utakatifu - ni matokeo ya utakaso. Ni hali ya neema na usafi ambayo utimilifu wa kufanana na Kristo hupendekezwa na kufuatwa (Wathesalonike 4:7) ... "muwe watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu' (1 Petero 1: 15,16), Tafuteni kwa bidii kuwa na Amani na watu wote, na huo utakatifu ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao" (Wahebrania 12:4; Luka, 1:74,75; 2Wakorintho 7:1; Tito 2:11,12; Waefeso 1:4; 4:13,24). Paulo alieleza pendekezo lake la'"kuleta kila mtu mtimilifu kwa Kristo." Kristo analirudia kanisa lililojaa utukufu na utakatifu; lisilo na hila wala kunyanzi wala Iolote kama hayo" (Waefeso 5:27; Zaburi 45:9-13).

**NEEMA TEKELEZI .**

**Urejesho** - ni kurudisha kitu kilichochukuliwa kwa njia isiyo ya haki, ama kutosheleza mtu aliyekosewa (Mathayo 3:8; Luka 19:8,9). Tendo hili pekee haliokowi, bali linaleta thibitisho kwa roho iliyofanya toba ya kweli. Urejesho unahimidi neema ya Mungu na kuhimiza ushuhuda ya mwumini. Pia hutoa nafasi ya upatanisho kwa waliokosewa. Ni kutimiza sheria ya upendo (Warumi 13:8). Baadhi ya marejesho yanafaa kufanywa kwa Uangalifu na chini ya uongozi wa mchungaji ili kuepusha chukizo au madhara zaidi.

**Sabato** - inamaanisha pumziko. Kuzingatia Sabato katika Agano 1a kale (siku ya saba) iliwekwa kusimamia mapumziko ya kiroho ya waumini ndani ya Kristo katika Agano Jipya. Hitaji ya Agano 1a kale ya kuzingatia Sabato sasa imezidiwa na amri "'muwe watakatifu," kwani katika Kristo mwumini anawezeshwa na kutakiwa kuishi kwa utakatifu kila siku. Jumapili sio Sabato bali ni siku iliyotengwa na Kanisa kuwa maalum ya ibada kwa Mungu na ushirika wa watakatifu (Hosea 2: 11; Wakolosai 2: 16, 17 Warumi 14:5,6; Waebrania 4:1-11).

**Vyakula na Vinywaji**-kukataliwa kwa baadhi ya vyakula na vinywaji katika Agano la kale hakikuendelezwa katika kanisa la Agano Jipya Mambo haya ya sherehe katika sheria ya Musa yalisulubishwa katika msalaba wa Kristo na kuondolewa kwenye Agano la neema (Wakolosai 2:13-17; Waefeso 2:15; Waebrania 9:8-11). Kile ambacho mtu hula na kunywa (mbali na yanayolewesha) ni jambo la dhamira wala hayaharibu kanuni ya ufalme wa Mungu (Warumi 14:17). Hata hivyo mtu lazima ajiadhari agizo la kiroho "chochote mfanyapo fanyeni kwa utukufu wa Mungu" (Warumi 14:2; 1 Wakorintho 8:8; Timotheo 4:1-5).

**Fungu la kumi** - Kutoa fungu la kumi inamaanisha kutoa moja ya kumi ya mapato ya mtu kwa Kristo - kuhani wetu mkuu. Ilianza kama tendo la hiyari na Ibrahimu, ilihitajika chini ya sheria ya Musa, na iliende1ezwa na Kristo kama sheria katika kanisa la Agano Jipya (Mathayo23: 23). Fungu la kumi inaletwa katika nyumba ya Mungu na kugawanywa ipasavyo na watumishi wanaolinda hazina (Malaki 3:10), Matoleo ya hiari yafaa kuhimizwa na yanachukuliwa kama zawadi kutoka moyoni. Fungu 1a kumi na matoleo kanisani ni sehemu ya mpango wa Mungu kusaidia kifedha kueneza kazi yake ulimwenguni kupitia kanisa. Tunatakiwa kwenye maandiko kuwa ‘walinzi wema wa kile Mungu ameweka chini yetu (Mwanzo 14:18 - 20-; Luka 11:42; l Wakorintho 16:2; 2 Wakorintho 9:6-9; Waebrania 7:1-21).

**Kiapo na maneno ya chukizo** – Kula kiapo ni kinyume cha roho ya Agano Jipya. "Lakini zaidi ya yote ndugu zangu, msiape, wala kwa mbingu, wala kwa nchi; wala kwa kiapo kingine chochote; bali ndiyo yenu na iwe ndiyo, na siyo yenu iwe siyo, msije mkaangukia hukumu" ( Yakobo 5:12). Yesu aIisema "Lakini mimi nawaambia, msiape kabisa; bali maneno yenu yawe ndiyo, ndiyo; sivyo, sivyo, kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu" (Mathayo 5:34, 37,Tazama kutoka 20:7). Himizo wa ukweli umetosha; umekubalika hata katika mahakama za kiulimwengu. Vivyo hivyo maneno

ya chukizo yanaangaza moyo usio safi wala haina nafasi katika maisha ya mwana wa Mungu (Mathayo 5:18,19; Wafilipi 1:27; 3:2; I Petro 1 :15; 2 Petro 2:7; Yakobo 3:8-10).

**Vinywaji na madawa ya kulevya**- "Mvinyo hudhihaki na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima" (Methali 20: 1). Maandiko yafundisha dhidi ya unywaji wa pombe ama vinywaji vingine vinavyolewesha kwa sababu Mungu ametuita katika kiasi timilifu (l Petro 5:8; l Wathesalonike 5:6; I Timotheo 3:2; Tito 2:2). Waumini wameonywa wasi "mpe shetani nafasi". kinachoitwa "Unywaji wa kiasi" au unaokubalika na watu hutoa nafasi kwa adui hivyo inafaa mwumini aache kabisa. (Waefeso 4:27; lsaya 28:7; l Wakorintho 5:11;6:10; Wagalatia 5:21). Mengi ya mambo yanayosemwa kuhusu vinywaji vya kulewesha,yanatendeka hata kwa madawa ya kulevya· Matumizi ya madawa kama tumbako, bangi, kokeni, n.k hunajisi mwili na hayaambatani na mafundisho na kanuni ya Kristo na maandiko. Vitu hivi vinanajisi mwili na kupinga mwito wa Mungu wa kuwa na kiasi (2 Wakorintho 7:1; Isaya 52:2; I Wakorintho 10:31,32; Waefeso 5:3-8; Yakobo 1: 21). Madawa ya matibabu yanafaa kutumiwa kulingana na maagizo ya daktari na tena kwa dhamira ulio nzuri.

**Bahati na sibu** - Maana na matokeo ya bahati na sibu imeelezwa vizuri katika maandiko,(Exodus 20:17; Mathew 6:11-13, 19-21; 1 Timothy 6:9,10).Ni tendo la kishetani,ambalo huendana na ulafi na kukufuru.Hivyo, basi Kanisa iko kinyume na kila aina ya bahati nasibu na imekataza.Kubahatisha,kasino,kupingana katika michezo,mfano;mtu anamwambia mwenzake nikishinda utanipa kitu Fulani nawe ukishinda nitakupa kitu Fulani.bahati nasibu ya kwenye mtandao,bingo,n.k.

**Nira Usio Sawa** - Biblia hufundisha wana wa Mungu kutofungwa nira moja na wasioamini. Kufungwa pamoja na wasioamini kwa muungano na vikundi vya kisiri na kula kiapo ni kinyume na mafundisho 1aini ya maandiko (2Wakorintho 9:14 - 17). Kama bi harusi aliyeposwa na Kristo, tunaahidi kuwa na utiifu usiogawanyika kwa Kristo. "Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu, Kwa kuwa niliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi." (2 Wakorintho 11:2; Yeremia 50:5). Kuwa mwanachama katika muungano ambayo inahitaji kiapo ya kulinda siri yapaswa kuvunjwa kabla ya kuwa mshirika wa kanisa. Yesu akajibu "Mimi nimesema na ulimwengu waziwazi;siku zote nilifundisha katika sinagogi na katika hekalu, wakusanyapo wayahudi wote; wala kwa siri mimi sikusema lolote" (Yohana18:20).

## KUBATIZWA KWA ROHO NA KARAMA ZA ROHO.

**Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu**- Ni tukio linalotendeka papohapo kwa muumini baada ya utakaso. Katika ubatizo huu, Kristo ndiye mbatizaji huku roho anapokelewa (Ms 3:11). Ubatizo wa Roho mtakatifu katika maisha iliyo takaswa unaambatana na kunena kwa ndimi. "Wote wakajazwa na Roho mtakatifu, na wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyo wajalia kutamka." (Matendo 2:2-4; 10:44-47; 19:1-60. Ubatizo wa Roho ni ubatizo wa kutiwa nguvu kiroho kuhudumu katika ufalme wa Mungu (Luka 24:49; Yohana 15:26: Matendo 1:8); pia unawezesha mtu kuhudumu

kikamilifu kanisani kwa juhudi ya kukuza mwili mwenyewe (1 Wakorintho 12:12 –28; Waefeso 4:11 –16).

**Kunena kwa ndimi** – kila mara huenda moja kwa moja na kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Muumini hunena kwa ndimi isiyojulikana; "vile Roho anavyoleta tamko" (Matendo : 2:4). "Ndimi usiyojulikana" hutofautishwa na kipawa cha Roho cha kunena kwa lugha mbali mbali" yaani kwa lugha zinazojulikana kwa binadamu. (Matendo: 2:6, 1 Wakorintho: 12:10, 14:2). Katika zote mbili (Ndimi isiyojulikana ama lugha inayojulikana kwa binadamu) lazima iwe kulingana na neno la Mungu (1 Wakorintho: 14:26). Kipawa cha kunena Kwa ndimi ni ishara kwa wasioamini (Matendo: 14:21 – 23), lakini inasaidia kwanza mwili wenyewe (Ms. 4).

**Karama za Roho:** - Kuna karama na kazi mbalimbali za Roho Mtakatifu (1Wakorintho: 12:4-11). Karama za Roho zilitenda katika Kanisa la Agano Jipya, lakini baadaye Kanisa likaanza kujitenga na dhihirisho za karama za Roho Mtakatifu zikaanza kudidimia. Baada ya kipindi cha kuasi imani katika karne ya nne na hata kwa "enzi za giza", katika historia ya ukristo, dhihirisho ya karama za Roho Mtakatifu (hasa kunena kwa lugha) karibu ilididimia. (Zilidhihirika kwenye sherehe hasa kati ya wakristo bandia wasio na imani inayokubalika). Nyakati hizi za mwisho (hasa tangu mwanzo wa karne ya ishirini) Mungu anamwaga Roho wake tena juu ya "wote wenye mwili" kulingana na utabiri; ili kutimiza mapenzi yake ya milele kupitia Kanisa (Yoeli: 2:28-32, 3:16-18, Matendo: 2:38-39).

**Ishara kufuata waumini:** - Ishara kufuata kwenye Agano Jipya zilinuiwa kuthibitisha neno la Mungu, na Yesu Kristo kama Mesia aliye ahidiwa. Waumini walipoendelea kutangaza neno katika jina la Yesu, Bwana alitenda pamoja nao na akashuhudia neno kwa ishara ikiwafuata (Mariko: 16:15-20). Ishara na miujiza zilifuata waumini ili kushuhudia utangazaji wa neno la Mungu, kushtaki roho za watenda dhambi kwa Mungu na kujenga mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12- 14).

**MAADHIMISHO:-**

**Ubatizo wa maji** - ni tendo 1a kuzamishwa ndani ya maji na mhudumu wa injili (Mchungaji, Askofu, Mwinjilisti), katika jina la Baba, jina la Mwana, na jina la Roho Mtakatifu. Imeagizwa na Kristo na Inaashiria kifo, kuzikwa na kufufuka kwake, inayoshuhudiwa katika maisha ya mwumini (Warumi 6:3-5) Adhimisho hili halina nguvu ya kusafisha dhambi bali ni ya dhamira safi kwake Mungu (1 Petro 3:21) ubatizo wa maji imekubaliwa tu kwa mtu aliyezaliwa mara ya pili (Mathayo 28:19; Mariko 1:8-10, 16:15,16; Yohana 3:22,23 Matendo 10:47,48; 16:33).Ubatizo wa maji hufananishwa na kufanywa upya kiroho; sio lango 1a kuingia kanisani.

**Meza ya Bwana** - Ni chakula cha ukumbusho wa jinsi Kristo alivyojitoa kama dhabibu na kutoa damu yake kwa aji1i yetu. Yesu aliagiza kushiriki katika meza hii takatifu kwa "Ukumbusho wangu"(l Wakorintho 11:24). Kumegwa kwa mkate usiotiwa chachu huwakilisha mwili wake; tunda 1a mzabibu (kinywaji kisichotiwa chachu) huwakilisha

damu yake. Adhimisho hii takatifu yafaa kufanywa Kwa hofu kubwa baada ya kujihoji (l Wakorintho 10:16-17; 11:23-30). Ni ishara ya nje ya Agano ya Kristo na kanisa (Luka 22:20).

**Kutawadha miguu** - Ni adhimisho kanisani. Kulingana Na kuadhimishwa kwa meza ya Bwana kristo alijifunga kitambaa, akaosha miguu ya mitume wake na akasema "Basi ikiwa mimi niliye Bwana na mwalimu, nitawatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadha miguu ninyi kwa ninyi" (Yohana13:14). Adhimisho hii inatofautishwa Na tamaduni ya Mashariki ya kati ya kutawadha miguu; Ina umuhimu Wa kiroho na imeagizwa kuadhimishwa na waumini (1 Timotheo 5: 10). Madhumuni ya kutawadha miguu halitimizwi kupitia upendo na kazi njema. Inatukumbusha kuwa tuna Bwana na mfalme mmoja ambaye ndiye kichwa cha kanisa, nasi sote ili tuwe watumishi wake, na watumishi kwa wenzetu

**UTAKATIFU WA KIUNGU.**

**Usafi wa maisha** - maisha ya binadamu ni takatifu kwa sababu ameumbwa katika mfano wa Mungu (Mwanzo 1 :27). Hivyo basi, kuchukua maisha isiyo na hatia haikubaliwi kamwe katika maandiko, pia utowaji wa mimba, kuuwa watoto wachanga, kudunga wagonjwa mahututi au wazee dawa ya kuuwa, mauwaji ya halaiki na kujinyonga. Usiuwe (Kutoka 20: 13). Yeyote atakayemwaga damu isiyo na hatia atachukuliwa kuwa na hatia mbele za Mungu (Mwanzo 9:6; Hesabu 35:30,31; Warumi 13:8-10; Ufunuo 21:8).

**Utakatifu Wa Ndoa** - Yesu alisema "Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye Na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawi1i watakuwa mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu; mwanadamu asiwatenganishe (Mathayo 19:4-6). Hivyo basi ndoa ni kati ya mume na mke hadi kifo (Waebrania 13:4). Uzinzi., uasherati, uvunjaji wa ndoa, kuowa ama kuolewa tena ni dhambi zinazo hujumu sheria za Mungu, na kudhuru nyumba na familia. Hata hivyo kutokuwa mwaminifu (kushirikiana kimapenzi nje ya ndoa) sio sababu ya kuvunja ndoa ama kuowa tena kwani "atakayeowa mke aliyeachwa na mumewe azini (Mathayo 19:19). Hivyo basi, wale wanaoowa au kuolewa tena kama waume au wake zao wa kwanza wako hai hawafai kuwa washirika kanisani.(Kutoka 20:14,17; Malaki 2:14-17; Mathayo 5:32 1Wakorintho5:1-5; 6:15-20; 7:2-3).

**Utakatifu Wa mwili**- Miili yetu ni hekalu ya roho mtakatifu, na tumeonywa kutukuza Mungu katika miili yetu (1 Wakorintho 6:20-21). Kama mtu akidharau hekalu 1a Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo" (1Wakorintho 3:16, 17). Pia tumeonywa kutoa miili yetu iwe dhabibu iliyo hai takatifu, ya kumpendeza Mungu (warumi 12:1), na "Fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" (1 wakorintho 10:31). Ushirikiano wa kimapenzi kati ya watu wa jinsia moja, imekatazwa kwenye maandiko. Matendo haya ni chukizo kwa Bwana, ingawa yaweza kukubaliwa na serikali ama kikundi cha kidini (Warumi 1:24-28, Mambo ya walawi 18:22,23;20:10 - 21). Mambo Kama kuchora mwili, kuchanja na

kuharibu mwili yana misingi ya kikafiri na yanapinga Roho wa utakatifu na mafundisho ya Biblia. Mambo haya hayafai katika maisha ya waumini (l Timotheo 2:8-10; Warumi I2:1,2; Isaya 3:16-22; l Yohana 2:15-17).

## ESKATOLOJIA

**Kurudi mara ya pili kwa Kristo kabla ya Milenia** - Kristo atarudi tena mawinguni kwa nguvu na utukufu mwingi (Mathayo 24:27,28) "Nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa  kwanza, kisha sisi tuliohai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu,, ili tum1aki Bwana hewani, na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele" (l Wakorintho 4:16-18; Tazama pia l Wakorintho 15:51,52).

**Unyakuzi:**
Wote (watakaonyakuliwa) katika ufufuo wa kwanza watahudhuria katika karamu ya harusi ya mwana kondoo (Ufunuo 19:7-9). Ndipo Kristo atarudi ulimwenguni kutawala pamoja na watakatifu miaka elfu moja (Ufunuo 19:4, 6; Zakaria 14:4,5;1 Wathesalonike 4:14; Yuda 14,15; Ufunuo 5:10; 19:11-21).

**Ufufuo** – kutakuwa na ufufuo kwa walio haki na wasio haki pia. Wenye haki watafufuliwa kwanza mara tu Kristo atakapotokea mawinguni kwa utukufu wake. Ufufuo wa waovu utakuwa baada ya miaka elfu moja ya utawala wa Kristo ulimwenguni. "Nina tumaini kwa Mungu, ambao hata hao nao wanalitazama, ya kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia." (Matendo 24:15; Daniel l2: 2; Ufunuo 20:4-6,41-58).

**Uzima Wa milele kwa wenye haki** - Dhawabu ya wenye haki ni uzima wa milele katika uwepo wa Mungu. "Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele, bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele" (Mathayo 25: 46; Luka 18:29,30; Yohana 10:28; Warumi 6:22; 1Yohana 5:11-13).

**Adhabu ya milele Kwa waovu** - wanaokataa na kupuuza mwito wa toba na wokovu wamewekewa hukumu wa milele (Yohana 3:15.-21). Jehanamu hakuna kuponyoka, hakuna kukombolewa, wala kumalizwa katika mauti. Jehanamu ndiyo "mauti ya pili," na ni mahala pa maumivu ya milele. "Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauwaji, na wazinzi, na wachawi na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika ile ziwa, liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili (Ufunuo 21:8; 20:10-15; 2 Wathesa1onike 1 :7-10; Yuda 14,5; Mathayo 25:46; Mariko3:29).

## MAFUNDISHO TEKELEZI  NA NIDHAMU Y A MKRISTO.

Maelezo yafuatayo yamefunuliwa wazi kwenye maandiko ama yanaambatana na mafundisho ya BibIia. Yamejulishwa kwetu kuhimiza uhusiano wetu na Kristo pamoja na ya wenzetu, na pia kutuhimiza katika njia inayoleta utukufu kwa jina la Kristo , na

kudhihirisha ushuhuda wa kanisa. Tumeonywa kwenye maandiko "'Bali uwe kielelezo kwa waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi "(1 Timotheo 4:12b). Yesu akaagiza "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" (Mathayo 5:16).

**Maombi** - Agizo laYesu ya "kesheni, mwombe" (Mathayo 26:41) haikuwa ya dharura Kama ilivyo Leo. Tunaishi katika "Nyakati mbaya," naye Kristo na mitume walituonya kuwa wakati utazidi kuwa mbaya inapokaribia kurudi kwa Bwana. Hivyo basi maombi ya kila siku na ibada ya familia yafaa kupewa nafasi ya kwanza katika kanisa la nyumbani. Kudumisha hali ya maombi ni funguo la kiroho kwa mtu binafsi na kwa kanisa lake. Kisha Yesu akasema "imewapasa kumwomba Mungu siku zote wala msikate tamaa" (Luka 18:1a) na mtume akawahimiza waumini "Ombeni bila kukoma"(1 Wathesalonike 5: 17). Pia tumeunganishwa katika "kuombeana (Yakobo 5:16,9). Maombi yafanywe kwa wafalme na wenye mamlaka na kwa walijitolea maisha yao kwa kazi ya Mungu na kwa huduma ya neno (1Timotheo 2:1-3). Maombi ni muhimu katika maisha ya kanisa kiasi kwamba kanisa linaitwa "Nyumba ya sala" (Isaya 56:7; Mathayo 21:13).

**Kusoma Biblia** - kusoma na kuelewa Biblia ni ya dhamana kwa vita vya kiroho kwa mwana wa Mungu. Kila mshirika kanisani amehimizwa kuwa mwanafunzi mwaminifu wa Neno takatifu la Mungu. Paulo anatuagiza "Jitahidi" kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu"(2 Timotheo 2: 15). Zaidi anasema "Ki1a andiko lenye pumzi ya Mungu yafaa kwa mafundisho, kwa kuonya, kwa kurekebisha na kwa kuagiza katika haki" (Ms 16). Umuhimu wa Neno la Mungu imedhihirishwa na mwandishi wa Zaburi "Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu, moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutendea dhambi (Zaburi 119: 10,11)

**Mahudhurio ya kanisani na kuabudu** - Ibada na ushirika pamoja na waumini, hasa waliopokea imani moja sawa nasi," ni jambo la muhimu maishani mwa mkristo. Ibada inafaa kuhisiwa moyoni na kuwa katika Roho, na iambatane na neno la Mungu (Yohana 4:23, Waefeso 5:19) Kila mshirika kanisani ni kiungo cha mwili wa Kristo, hivyo kanisa litazuiliwa kwa kiwango cha mtu mmoja kukosa kutimiza mwito wake. Kama kawaida waumini wafaa kuunga mkono kila kazi ya kanisa, na kujumuika kikamilifu. Onyo la mwandishi wa kitabu cha Waebrania yatupasa kuzingatia "Wala tusiache kusanyika, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia" (Waebrania 10:25). Watoto wapewe maagizo nyumbani, na wafundishwe kwa amri na mifano kuheshimu nyumba ya Mungu.. Wahudumu na familia zao wawe mifano katika maisha na maongezi yao. " Nao watafundisha watu wangu tofauti uliopo kati ya vitu vitakatifu na vitu vya siku zote, na kuwafundisha kupambanua kati ya yaliyo mabaya na yalio mema" (Ezakieli 44:23a).
Hali ya maombi inaleta mazingira yafaayo ya ibada na huduma ya neno la Mungu. Inafaa waumini kuzidi katika maombi huku wahudumu wakitoa ujumbe, la sivyo shetani atakuja na kuiba neno la Mungu moyoni mwao (Mariko: 4:4, 15).
Upendo wa Mungu "Umeangaza moyoni mwetu na Roho Mtakatifu" inafaa ajaze

mazingira yetu ya ibada. Upendo Na utawale matendo yetu yote Na kuonekana Kwa kila mtu bila upendeleo (1 Wakorintho 13). Tunahitajika kuwa waangalifu katika kuonyesha upendo kwa wageni. Yesu alisema "hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi" (Yohana 13:35).

**Kutembea kwa uangalifu:-** Wana wa Mungu na "waenende kwa uangalifu; si kama watu wasio na hekima, bali kama watu wenye hekima; mkikomboa wakati kwa maana zama hizi ni za uovu" (Waefeso 5:15,16). Kuishi maisha ya utaua nyumbani na ugenini haitaacha nafasi ya watu kukufikiria ama kukusengenya kwa unafiki. Maisha yetu yanafaa kuwa takatifu katika neno na katika tendo kama inavyofaa mwana wa Mungu. Kama mwakilishi wa Kristo katika ulimwengu, washirika wa Kanisa la Mungu, tujipambe kwa mavazi ya kusitiri na moyo wa kiasi (Zaburi:1:1-3; Wafilipi:1:27; 1 Wathesalonike:5:5-23).

**Burudani na mvuto wa ulimwengu:-** Wakristo hawafai kuhusika katika viburudisho na mapambo ya ulimwengu ambapo sheria ya Utakatifu unabadilishwa. Waumini watangamane na wasio amini chini ya mpangilio mwafaka, la sivyo mtu akanaswa kwenye mtego wa shetani. "Muwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi; kama simba angurumae, huzungukazunguka akitafuta mtu ammeze" (1 Petero 5:8, 2 Petero 2:19-22).

**Uhusiano mbaya:** Paulo anatuonya "wala msimpe ibilisi nafasi" (Waefeso 4: 27). Kuwa na uhusiano wa karibu sana na mtu wa jinsia tofauti, hata kama ni ndugu au dada katika Bwana, unaleta mazingira ya majaribio na hutoa nafasi kwa "Hila za shetani". Samsoni ni mfano wa tabia hii isiyo ya hekima, iliyomsababisha kuanguka kutoka kwa neema (Waamuzi 16), huku Yusufu kwa hekima aliponyoka hali hii (Mwanazo 39). Labda Paulo alikuwa na Yusufu akilini mwake alipoonya "Ikimbieni zinaa" (1 Wakorintho 6:12). Maneno ya Yakobo nduguye Bwana, pia yalikuja akilini, "Halafu ile tamaa ikiisha kuchukuwa mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti" (Yakobo 1:13-15). Kwa kuzingatia maonyo haya, uangalifu unahitajika ili kuepusha uhusiano na hali inayoweza kumnajisi mtu na kuleta matusi kwa Kristo na kanisa.

**Mapambo ya nje:-** Wakristo ni mabalozi wa Kristo katika ulimwengu wa zama hizi (2Wakorintho 5:20). Kwa hivyo inawapasa kujipamba Kama inavyostahili kawaida na usafi wa Bwana wao. Kujipamba kulingana na mtindo wa kiulimwengu ulio na kujipodoa usoni, dhahabu, lulu, nguo za thamani, n.k. Hayaambatani Na ushuhuda wa mtu aliyemtambua Mungu. "Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu na kuvalia mavazi… bali muwe na utu wa moyoni usio onekana, katika mapambo yasiyo haribika; yaani roho ya upole na utulivu; iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu" (1 Petero 3:1-6; 1Timotheo 2:8-10; Isaya 3:16-24; 61:10).

**Heshima kwa jumuiya na kwa mtu binafsi**:- Kujihoji na kukadiri imani ya mmoja na hali ya kiroho ni swari (1 Wakorintho 11:28). Kujali wengine Kwa moyo wa dhati ni nzuri na umehimizwa. Sisi ni wachungaji wa ndugu zetu. Ushauru inatolewa tu katika

roho ya upendo na kwa hekima ya Mungu, na chini ya sheria na nidhamu iliyoandikwa katika injili (Mathayo 18:15-20). Moyo mkali wa kukosoa unadhuru kukuwa kiroho kwa mkosoaji mwenyewe na pia anaye kosolewa: (Mathayo 7:1-5; 2 Wakorintho 2:1-11; Wagalatia 5:14, 15; Waefeso 4:30-32). Adhabu na itolewe tu kama suluhisho ya mwisho, na kila mara katika ushauri wa kimaombi unaokusudia wema wa anayeadhibiwa (1 Wakorintho 5:1-7; Wagalatia 6:1-5).